# JARIBIO LA MTIHANI WA AIM PRESS

# 8 DARASA LA NANE - MWAKA 2021

# KISWAHILI : LUGHA

**MUDA: SAA1 DAK.40**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze nafasi zilizo wazi 1 - 15.***

Ulaji wa __1__ ni jambo lililoshamiri kabisa __2__ jamii ya Wakenya. Watu wengi bado __3__ ulaji rushwa ulivyo na __4__ makubwa katika jamii. Ulaji rushwa unapoenea kwa __5__ ambacho umefika hapa __6__ huwa ni __7__ sana kwa wananchi kupata huduma __8__ pasipo kuzunguka mbuyu! Hebu __9__ ni uchungu ulioje, kwa majeruhi wa ajali __10__ kwenye fomu kwa kukosa mtu wa __11__! Kisa na maana? Ati hana __12__ za kuhonga! Kwa tamaa ya pesa __13__ kwamba, maskini wa Mungu ni __14__ hajijui wala hajitambui! Watu wengine hula rushwa huku wakidai eti, __15__ wanayolipwa haitoshi chochote. Huo kwa kweli ni upuuzi.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. pesa | B. rushwa | C. chai | D. karata |
| 2. | A. miongoni | B. ndani | C. katika | D. kunako |
| 3. | A. hawatambui | B. kuona | C. kusikia | D. hawajadhani |
| 4. | A. matokeo | B. hasara | C. maswali | D. madhara |
| 5. | A. kiini | B. kasi | C. kipimo | D. kiwango |
| 6. | A. mashambani | B. kijijini | C. mijini | D. nchini |
| 7. | A. vigumu | B. haraka | C. rahisi | D. wapesi |
| 8. | A. zozote | B. popote | C. lolote | D. kokote |
| 9. | A. nambie | B. tafakari | C. tazama | D. sikiliza |
| 10. | A. kufika | B. mbaya | C. kufia | D. kukaa |
| 11. | A. kumshauri | B. kumwongola | C. kumhudumia | D. kumtwaa |
| 12. | A. fedha | B. vito | C. rushwa | D. mali |
| 13. | A. haujulikani | B. hatambulikani | C. hatujui | D. haitambuliwi |
| 14. | A. mchovu | B. tabaani | C. mahututi | D. hoihoi |
| 15. | A. marupurupu | B. ujira | C. mapato | D. mishahara |

***Chagua jibu lifaalo katika nambari 16 - 30.***

16. Mizigo ilitumbukizwa majini ______ ikazama ______
    A. chubwi / ji B. tifu / ji
    C. pu / ji D. chubwi / zii
17. Kanusha maneno haya.
    Wangejikinga wangenusurika.
    A. Hawangejikinga hawangenusurika
    B. Wasingejikinga wasingenusurika
    C. Wangejikinga hawangenusurika
    D. Wangejikinga wasingenusurika
18. Fahari ni kwa mori ilhali beberu ni kwa ______
    A. mbarika B. pora C. jike D. tembe
19. Jaza pengo zifuatazo.
    Kutokana na kifo cha ______ wao ______ walipatwa na ______
    A. masahibu, mashaibu, masaibu
    B. masahibu, masaibu, mashaibu
    C. masaibu, masahibu, mashaibu
    D. masaibu, mashaibu, masahibu
20. Chagua methali yenye maana sawa na:
    Aliye juu mngojee chini.
    A. Mpanda ngazi hushuka
    B. Jungu kuu halikosi ukoko
    C. Aliye kando haangukiwi na mti
    D. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe
21. Chagua kundi la vitenzi.
    A. Chora, funga, aka, koroma
    B. Mnene, mrefu, mweusi, laini
    C. Mwizi, kasha, jambazi, jangili
    D. Vyema, haraka haraka, vibaya, polepole
22. Mwalimu mkuu alikuwa amebeba **barua nyingi**.
    Maana ya maneno yaliyopigwa mstari ni ______
    A. kipeto B. tita C. korija D. koja
23. Mke wa mjomba huitwa ______
    A. mkaza B. mkazahau
    C. mkwarima D. mbiomba
24. Andika wingi wa sentensi hii.
    Mti uzao embe unaitwa mwembe.
    A. Miti zizaayo miembe zinaitwa maembe
    B. Miti izaayo miembe huitwa nyembe
    C. Mti izaayo maembe huitwa nyembe
    D. Miti izaayo maembe inaitwa miembe
25. Ng'ombe ______ mjombangu ______ maziwa ______
    A. ya, na, mengi B. ya, ana, mengi
    C. wa, ana, nyingi D. wa, ana, mengi

26. Sentensi iliyo katika wakati timilifu ni ________
A. Nende shuleni
B. Aende shuleni
C. Ameenda shuleni
D. Ataenda shuleni

27. Mwalimu alikuwa hana budi kurudi nyumbani. Je, alirudi nyumbani?
A. Ndiyo
B. Hapana
C. Labda
D. Haijulikani

28. Andika kwa udogo.
Mtoto yule mdogo analia.
A. Kitoto kile kidogo kinalia
B. Mtoto yule kidogo analia
C. Kitoto yule mdogo analia
D. Kitoto kile kidogo analia

29. Kwa katika sentensi hii imetumiwa kumaanisha nini?
Alikuwa balozi kwa miaka saba.
A. Kulingana
B. Sababu
C. Wakati
D. Mahali

30. Akija mtu ________ ritampa chandarua ________
A. mwingine, kingine
B. mwingine, nyingine
C. mwengine, ingine
D. mwengine, jingine

**_Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31 - 40._**

Nilizaliwa na kulelewa katika familia iliyotajika. Baba yangu Mlajasho alikuwa tajiri wa mali na moyo. Mimi na ndugu yangu mdogo hatukujua maana ya uhitaji kwani baba alitukidhia mahitaji yetu yote. Nyumbani mwetu kila siku mlishiba na kutapika watu wa kila sampuli waliokuja kulilia hali kwa baba. Baba aliwakidhia kwa mengi. Kuna waliopewa ruzuku mbalimbali za vyakula, kuna waliopewa vibarua mashambani au kazi pale nyumbani.

Almuradi kila mwanakijiji alifaidika kutokana na mkonowazi wa baba. **_Ndugu yangu mdogo hakuishi kuwabughudhi waja hawa na kuwaita waegemea nundu_**.

Siku zilisonga na kupita kama maji ya mto. Hata nikajipata katika shule ya msingi. Niliyakumbatia masomo yangu kwa hamu kubwa. Sikuwa na wakati wa kufanya ajizi. Kwani baba pamoja na pato lake nono hakuwahi kudekeza hisia za ugoigoi. Nasi ilibidi tufuate nyayo zake, kwani mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina. Nilifanya mtihani wangu wa darasa la nane na kuvuna nilichopanda. Asubuhi baada ya kutangazwa kwa matokeo ya mtihani huo niliamshwa na sauti ya, "Pongezi mwanangu," kutoka kwa baba. Baba alikuwa amebeba gazeti la siku hiyo, usoni amevaa tabasamu kubwa. Sikuamini maneno yake. Nilimnyang'anya gazeti na ikawa kweli mwenye macho haambiwi tazama. Nilikuwa mwanafunzi bora nchini. Nilijiunga na shule mojawapo ya kitaifa.

Siku nilipovuka kizingiti cha lango la shule ya kitaifa ya **_Tindi ndipo maisha yangu yalipoanza kuingia ufa_**. Nilikutana na Tamasha, mwanafunzi mchangamfu na mcheshi. Alijitambulisha kuwa alisoma shule iliyokuwa jirani na ile yangu ya msingi. Urafiki shakiki ukatawala kati yake nami. Tulikuwa daima tunaandamana. Hayo hayakunitia shaka, kwani Tamasha, alinihimiza kila mara nitie bidii masomoni. Hata hivyo, siku zilivyosonga ndivyo tabia yake halisi ilivyonibainikia.

Jioni moja Tamasha alikuja chumbani mwangu akiwa amebeba unga aliouita dawa ya homa. Aliniambia nijaribu kutibu homa ambayo ilikuwa imenikaba kwa siku ayami. Nami, kwa kutomvunja rafiki yangu, nikachukua unga huo na kuutia kinywani, ingawa kwa kweli mwalimu wetu alikuwa ametuonya dhidi ya kutumia dawa zozote bila maelekezo ya daktari. Unga huu haukuitibu homa yangu ila ulinipa utulivu mkubwa wa akili, utulivu ambao sikuwa nimewahi kuushuhudia maishani.

**_Uzuri wake huu ni wa mkakasi tu_**? "Nilijiuliza." Laiti ningalijua. Hata hivyo maswali yote haya hayakuwa na faida tena. Nilikuwa tayari nimezama katika tatizo sugu la matumizi ya dawa za kulevya.

Nilijisuta moyoni kwa matumizi ya dawa za kulevya ambayo yalielekea kuyagongesha mwamba maisha

yangu shuleni. Hata hivyo haikuwa rahisi kuacha kwani nilichelea kuitwa limbukeni na wenzangu. Matokeo ya haya yote yakawa kuzorota kwa masomo yangu. Walimu hawakuchelewa kuona mabadiliko yaliyonikumba. Walijaribu kunishauri na kutaka kujua kilichokuwa kikinisumbua. Walipoona kwamba hali yangu haikubadilika na kwamba nimeshindwa kuwaambia tatizo langu, walimjulisha mwalimu mkuu ambaye hakukawia kumwita baba.

Mazungumzo kati ya baba na mwalimu mkuu yalinitia fadhaa kubwa kwani sikutaka kuwaambia nilitumia dawa za kulevya, ingawa kwa kweli mwalimu mkuu alishuku. Walijaribu kunishika sikio kuhusiana na tabia hii yangu lakini tangu lini **sikio la kufa** likasikia dawa? Niliendelea na uraibu wangu hadi siku nilipofunzwa na ulimwengu baada ya kufumaniwa na naibu wa mkuu wa shule mjini nikipiga maji. Nilipewa adhabu niliyotarajia. Nilijipata nyumbani kwa muda wa mwezi mzima nikiuguza vidonda vya moyo na akili. Kijiji kizima kilijua nimefukuzwa shule kwa sababu ya matumizi ya dawa za kulevya. Sikuwa na pa kuutia uso wangu. Hata hivyo hili lilikuwa funzo kubwa kwangu.

Mama yangu aliweza kunipa nasaha na kunishauri niache kutumia dawa hizo. Mara hii maneno aliyoniambia yalikuwa na maana. Niliyasikiliza kwa makini, hata baba alipopata barua kumwarifu aniregeshe shule, nilikuwa tayari nimeamua kujiunga na chama cha vijana wanaopigana na matumizi mabaya ya dawa shuleni.

31. Mambo yanayoonyesha kuwa Mlajasho alikuwa tajiri wa mali na moyo ni ______
  A. kukidhi mahitaji ya wana, kuwapa watu riziki
  B. kukidhi mahitaji ya wana, watu kumlilia hali
  C. kukidhi mahitaji ya wana, watu kujaa kwake
  D. kukidhi mahitaji ya wana, kumkana mwanawe

32. "Ndugu yangu mdogo hakuishi kuwabughudhi waja hawa na kuwaita waegemea nundu?" Hii inaonyesha ndugu mdogo alikuwa ______
  A. Mwenye kujisifu  B. Mwenye uzushi
  C. Mwenye mapuuza  D. Mwenye uchoyo

33. Msimulizi alisoma kwa hamu kwa kuwa ______
  A. baba yake alikuwa mwenye bidii
  B. alipenda masomo yake
  C. alitaka kufuata nyayo za ndugu yake
  D. Baba yake alikuwa mkali

34. Kifungu "ndipo maisha yangu yalipoanza kuingia ufa" kinamaanisha
  A. maisha ya msimulizi yalianza kubadilika
  B. maisha ya msimulizi yaliharibika
  C. maisha ya msimulizi yalianza kupata matatizo
  D. maisha ya msimulizi yaliporomoka

35. Msimulizi hakutaka kuacha "unga" kwa sababu ______
  A. hakutaka kumuudhi Tamasha
  B. alikuwa amezoea uraibu kwa kamaliza
  C. alichelea kudunishwa na wenzake
  D. tayari alikuwa mraibu

36. Mambo yanayoonyesha kuwa kifungu hiki kinapinga matumizi ya dawa za kulevya ni ______
  A. msimulizi kufukuzwa shule, msimulizi kujiunga na wanaopinga matumizi mabaya ya dawa shuleni
  B. walimu kumshauri msimulizi, mama pamoja na mwalimu mkuu kumwonya msimulizi shuleni
  C. msimulizi kuacha kuuza dawa, mama kumshauri msimulizi
  D. walimu kugundua tatizo la msimulizi, kumshauri msimulizi

37. Kulingana na kifungu hiki jamii inakabiliana na tatizo la matumizi mabaya ya dawa kwa ______
  A. ushirikiano kati ya wazazi na walimu na kuwajibika kwa vijana
  B. kuwapeleka watoto shuleni, matajiri kuwasaidia watu
  C. ushirikiano kati ya wazazi na walimu kuaibika kwa vijana
  D. wazazi kwenda shuleni wanapoitwa

38. Methali ambayo **haifai** kujumlisha ujumbe wa taarifa hii ni ______
  A. Mchezea tope humrukia
  B. Nazi mbovu harabu ya nzima
  C. Mwegemea nundu haachi kunona
  D. Mchovya asali hachovyi mara moja

39. "Uzuri wake huu ni wa mkakasi tu?" Ina maana ______
  A. alikuwa mnafiki
  B. alikuwa mcheshi
  C. hakuweza kutegemeka
  D. hakuweza kuaminika

40. Msimulizi alikuwa "sikio la kufa" kwa sababu ______
  A. alifumaniwa na naibu wa mwalimu mkuu akipiga maji
  B. hakupona homa baada ya kutumia unga
  C. alipata adabu aliyotarajia baada ya kupiga maji
  D. hakuacha uraibu wake baada ya kuonywa na mwalimu

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Kuna maneno mengine ambayo yana maana zaidi na watu wengi huwa hawaoni. Kwa mfano neno "Nikaha." neno hili lina umuhimu usioweza kuonekana na waja wengi. Fikiria watu ambao ni tofauti kimila, kisura, kikabila na pengine kitaifa kukata shauri kuishi pamoja, kugawana walichonacho, kula pamoja, kuzungumza pamoja, kusaidiana kwa mema na hata kuvumiliana, si jambo la kawaida.

Si ajabu watu wakasema ni kufunga pingu za maisha kwani ni mkataba wa kuishi pamoja daima dawamu bila kuwa lila na fila kabla ya kuona marafiki huwa na uhuru wa kutembea, kula, kustarehe, kuvaa na kufanya lolote anaona linafaa. Si ajabu kuona kijana akivaa nguo zisizo na aibu. Wengine hulewa ovyoovyo bila kujali lolote.

Punde nikaha ifanywapo huwa mtu sasa huwa peke yake. Humlazimisha kurekebisha tabia yake yenye doa ili iambatane na matakwa ya mwenzake. Pia kila mmoja hana budi kuifikiria jamaa ya mwenzake ili heshima idumu. Heshima ya kivyele ni muhimu sana kwani huleta mshikamano katika jamii nzima. Ajabu ni kwamba heshima ya bavyaa huenda ikawa tofauti na ya bamkwe. Hivyo basi lazima kama ibada kujua mambo muhimu baada ya kuwa pamoja.

Kila kabila au nchi huwa na njia maalumu ambazo hufuatwa wakati wa kupanga mambo ya nikaha. Kuna wale hupendekeza vijana watafutane waoane, wengine ni lazima wazazi washirikishwe na wengine huozwa kwa watu wasiowajua. **Kwa hivyo mila na tamaduni ndizo huwa uti wa mgongo katika kila nikaha**.

Jinsi mvulana na msichana wanavyokutana pia huwa tofauti sana. Kuna wale hukutana njiani, sokoni, mtoni, kisimani au hata wakati wa kutafuta kuni. Wengine hupatana vyuoni wanapopata elimu ya juu. Si ajabu pia kuwa walionana wakati wa matanga, nikaha, ziarani ama wakati kuna mikutano mbalimbali. Watoto huwa wanaanza kuongea faraghani na mbegu za mapenzi huanza kuota polepole.

Siku hizi vijana wengi hukutana michezoni, likizoni au katika sherehe mbalimbali. Sherehe hizi zinaweza kuwa za shuleni, maabadini au hata kiamboni. Jambo muhimu ni kuwa mapenzi ya dhati huwafanya watu kuishi pamoja bila kuzozana. Tumeshuhudia vijana wengi wakijitoa uhai kwa sababu ya mapenzi machanga. Wanafunzi wote wanafaa kujua kuwa wao ni wachanga na mapenzi kwao ni sumu. Wasipojua haya watavingwa na wengine kuambukizwa magonjwa ya zinaa ambayo ni hatari.

41. Kulingana na aya ya kwanza ni kweli kusema kuwa ________
   A. watu wote huwa wa kabila moja katika nikaha
   B. vitawe ni maneno yenye maana zaidi ya moja
   C. maneno yote yana umuhimu ambao hauonekani
   D. nikaha na mambo yake ni jambo lisilo la kawaida

42. Msemo kukata shauri una maana gani?
   A. Kudakiza B. Kuamua
   C. Kusema D. Kugawa

43. Vijana hawawezi kuonana wapi kulingana na kifungu hiki?
   A. Wanaposafiri ziarani
   B. Wanaposoma vyuoni
   C. Wanapokunywa pombe
   D. Wanapocheza pamoja

44. Ni kwa nini nikaha huitwa pingu za maisha?
   A. Wanaoana hutarajiwa kuishi pamoja milele
   B. Watu huonywa dhidi ya kutoa talaka
   C. Kwa sababu wasimamizi hutoa ushahidi bora
   D. Waja wengi hushuhudia mkataba wa maisha

45. Neno nikaha lina maana zifuatazo ila
   A. Arusi B. Maarusi C. Ndoa D. Chuo

46. Ni kweli kusema kuwa ____
   A. si lazima kujua mambo muhimu wakati wa nikaha
   B. bamkwe na bavyaa huwa na mila moja
   C. matakwa ya watu wote huwa siku ya nikaha
   D. heshima ya wazazi wote huleta ushirikiano

47. .... **kwa hivyo mila na tamaduni ndizo huwa uti wa mgongo katika kila nikaha**. Kauli hii ina maana kuwa ________
   A. nikaha ni uti wa mgongo katika maisha
   B. mila na tamaduni hushikilia nikaha
   C. mila na tamaduni hazitangamani na nikaha
   D. tamaduni pekee ni muhimu kuliko nikaha

48. Jambo ambalo linashangaza katika aya ya tano ni ____
   A. kuongea faraghani kupanda mbegu
   B. watu kuenda matanga pamoja
   C. ziara kubadilika na kuwa nikaha
   D. vijana kujuana wakati wa nikaha

49. Upi si ugonjwa wa zinaa?
   A. Ukimwi B. Kisonono
   C. Kaswende D. Saratani

50. Wanafunzi watapatwa na maafa gani wakifanya mapenzi?
   A. Kupata mimba wakiwa wadogo
   B. Kuambukizana magonjwa ya zinaa
   C. Kupata sumu inayowapa mapenzi mengi
   D. Vijana kujitoa uhai na mapenzi